MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili: Uchunguzi wa Diwani ya Kurunzi

Davian Buguna*

*Idara ya Lugha na Stadi za Mawasiliano, Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania.*

## IKISIRI

Nafasi ya mwanamke katika jamii imeendelea kuwa muhimu kila siku. Mathalani watunzi wa kazi mbalimbali za fasihi wakiwemo wa ushairi wameendelea kumsawiri mwanamke katika kazi zao. Aidha, wahakiki wa kazi mbalimbali za fasihi wanaonesha kuwa diwani mbalimbali zilizotungwa hususani na watunzi wa kiume, zimemsawiri mwanamke kwa mtazamo duni sana ukilinganisha na mwanaume. Makala hii imechunguza usawiri wa mwanamke katika diwani iliyotungwa na mtunzi mwanamke.Uchunguzi huo umeongozwa na Nadharia ya Ufeministi. Data za makala hii zilipatikana katika Diwani ya Kurunzi ya Rose Mbijima kwa mbinu ya usomaji makini. Matokeo yanaonesha kuwa yapo maendeleo makubwa yaliyopigwa na mwanamke katika kujiondoa katika hadhi ya chini na hali duni, kama ambavyo anachorwa katika kazi nyingi za kifasihi. Data zinadhihirisha kuwa mtunzi amemchora mwanamke kwa kiasi kidogo katika mtazamo hasi hususani katika masuala ya mapenzi na ndoa kuakisi hali ilivyo katika jamii nyingi za kiafrika. Aidha, mtunzi mwanamke amemsawiri mwanamke katika mtazamo chanya kwa kiwango kikubwa. Mwanamke amesawiriwa kama mtu mwenye mtazamo wa kimapinduzi juu ya mambo mbalimbali yanayoendelea katika jamii, mwanamke ameonekana akipaza sauti na kutoa maoni yake. Makala hii, inahitimisha kwa kutoa mapendekezo kuwa, kazi za watunzi wa kike wa ushairi ziendele kutafitiwa ili kuchochea mabadiliko makubwa ya wanawake juu ya mtazamo hasi dhidi ya jinsi yao na jamii kwa ujumla kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii.

## KUHUSU MAKALA

*Maneno Muhimu:*
Mwanamke,
Nafasi ya Mwanamke,
Usawiri Hasi na Chanya,
Ushairi,
Watunzi.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 22 Decemba 2025
Tarehe ya Kurekebishwa: 2 Machi 2026
Tarehe ya Kukubalika: 21 Machi 2026
Mtandaoni: 8 Aprili 2026

## 1. Utangulizi

Nafasi ya mwanamke katika kazi za fasihi imeelezwa kwa mtazamo unaodhaniwa kuwa ni hasi na watunzi na wahakiki mbalimbali wa kazi za kifasihi (Kimondiu, 2019; Ngaiza, 2004). Wanawake wanaona kuwa wamesawiriwa katika kazi nyingi za kifasihi kwa mtazamo duni sana ikilinganishwa na mwanaume (Lyatuu, 2011). Indede (2011) anasema kwamba, jambo la kushangaza ambalo linaleta ugumu katika kujadili nafasi ya mwanamke kwa mtazamo mpana zaidi ni kuwa ushairi ambao umeandikwa na wanawake ni nadra sana na hasa katika enzi ya karne ya ishirini na moja. Mawazo haya ya Indede (2011) yana ukweli kwani kazi nyingi za ushairi ambazo zinatumika kuhakiki suala la nafasi ya mwanamke ni zile ambazo zimeandikwa na wanaume. Mawazo haya yanadhihirisha kuwa suala la nafasi ya mwanamke katika jamii halijatendewa haki katika mijadala, kwani tafiti nyingi na mijadala kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii imewapendelea watunzi wanaume na kuwanyanyapaa wanawake.

Aidha, Mwakanjuki (2022) anaeleza kuwa wahakiki wengi wa fasihi za Kiafrika wanakabiliana na wanawake katika miktadha mingi ya kiuhakiki, lakini wanakwepa kuhakiki uhusika wao kutokana na ujitokezaji wao katika taswira mbalimbali. Anaendelea kueleza kuwa baadhi yao wamemtazama mwanamke kama mfungwa anayewekwa ndani muda wote pasipo kupewa ruhusa ya kutoka nje. Hali hiyo inamfanya kukosa haki zake na uhuru wa kutembea kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Athari ya mtazamo huo zilimfanya Challigha (2011) kuwatazama wanawake kama kundi la watu ambalo limekandamizwa na kutengwa kwa muda mrefu bila kushirikishwa katika kumiliki mali. Hivyo, jitihada za dhati zinapaswa kufanyika kuhakikisha diwani zilizoandikwa na watunzi wanawake zinahakikiwa ili kuchunguza mtazamo wao kuhusu nafasi ya mwanamke. Aidha, upatikanaji wa diwani zilizoandikwa na watunzi wa kike bado ni mgumu hata katika karne hii ya 21. Hii pia husababisha kupunguza wigo wa uhakiki wa jinsi washairi wanawake wanavyowachora wanawake katika kazi zao. Mtunzi nguli, Profesa Mulokozi, katika dibaji ya kitabu hiki cha Kurunzi (2019), anabainisha kuwa ingawa watunzi wa mashairi wapo na wanazidi kuongezeka, changamoto ya uhaba wa wachapishaji wa mashairi nchini Tanzania ingali inaendelea. Anaendelea kusema

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: davian.buguna@mzumbe.ac.tz

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Buguna D. (2026). Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili: Uchunguzi wa Diwani ya Kurunzi. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(1), 1 – 8. https://doi.org/10.61889/baxmfs93.

© 2026 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

kuwa watunzi wa ushairi wa kijadi ni wengi na pia washairi wa bongo flava, na wachache wanaotunga ushairi huru au mavue. Pamoja na hayo, uchapishaji umeendelea kuwa changamoto.

Aidha, Abdalla (2020) alichunguza Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Kidumbaki Zanzibar. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha usawiri hasi na chanya wa mwanamke katika nyimbo za Kidumbaki. Mathalani kuhusu usawiri hasi, mwanamke amechorwa kama mtu asiyejisitiri, chombo kisicho thamani, kiumbe asiye huruma, mshirikina, mtu anayelaghaiwa kimapenzi, kiumbe hadaa na malaya. Usawiri chanya wa mwanamke katika Nyimbo za Kidumbaki umemchora mwanamke kama mlezi, mtiifu, mtu mwenye umbo zuri na jasiri. Matokeo ya utafiti wa Abdalla (2020) yanaonesha kuwa usawiri chanya wa mwanamke bado unahusisha sifa za kimaumbile na kibinadamu. Masuala kama ya umiliki wa uchumi na uongozi hayaonekani kuzungumziwa katika nyimbo za Kidumbaki, hali inayoonesha kuwa mwanamke bado yuko duni katika maeneo mengi muhimu.

Vilevile, Ali (2014) alitafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa watunzi wote wawili wanafanana katika kumsawiri mwanamke katika mashairi yao. Mathalani mwanamke amesawiriwa kama ni mlezi, chombo cha starehe, malaya na mwenye mapenzi ya dhati. Hata hivyo, matokeo haya yanatokana na uchunguzi uliofanyika katika mashairi yaliyotungwa na watunzi wanaume. Hivyo hatujui hali ilivyo katika mashairi yaliyotungwa na watunzi wanawake.

Kwa upande mwingine, Limbe (2024) alifanya utafiti kuhusu usawiri wa wanawake wenye uwezo katika Muziki wa Bongo Fleva nchini Tanzania. Katika matokeo, alieleza kuwa huenda kinachowainua wanaume katika jamii kuwa wenye uwezo na mamlaka ni nguvu za kiuchumi hususan fedha na elimu. Ijapokuwa kuhusu hili, Schipper (2006) anaeleza kuwa utamaduni wa jamii ungali unampa fursa zaidi mwanaume. Hii ikimaanisha kuwa licha ya sababu mbalimbali zinazoweza kuelezwa kuhusu nafasi na nguvu ya mwanaume katika jamii, hatuna budi kupuuza nafasi ya utamaduni wa jamii husika. Limbe (2024) anaendelea kueleza kuwa kupitia nyimbo za bongo fleva kama vile Narudi Kijijini, mwanaume asiye na fedha anaonekana kuwa na maisha duni, na unyonge kama ilivyo tu kwa wanawake wengi katika kazi za fasihi. Ilibainika kuwa mwanamke mwenye pesa anaweza kunyanyasa, kudhalilisha, kumnunua mwanamume na kumtumia kwa matakwa yake (Limbe, 2024)

Hii ni kusema kuwa tafiti nyingi tangulizi zimemsawiri mwanamke kwa mtazamo chanya na hasi katika kazi mbalimbali za utanzu wa ushairi. Kwa upande mmoja zimemsawiri mwanamke aliyejikomboa kiuchumi na kielimu, na kwa upande mwingine, mwanamke ambaye hajajikomboa katika nyanja za kiuchumi na kielimu, ambaye ni tegemezi kwa mwanaume. Hata hivyo, matokeo ya kazi hizi yanaacha ombwe kwa kuwa kazi zilizochunguzwa hazijahusisha mashairi yaliyotungwa na watunzi wanawake. Hivyo mtafiti aliona haja ya kufanyika utafiti zaidi kuhusiana na usawiri wa mwanamke katika ushairi ulioandikwa na mwanamke. Hivyo, makala hii itaongeza maarifa katika eneo hili kwa kuchunguza usawiri wa mwanamke katika mashairi yaliyotungwa na mtunzi mwanamke.

## 2. Nadharia ya Utafiti

Makala hii itatumia Nadharia ya Ufeministi. MacKinnon (1991) anaeleza kuwa Nadharia ya Ufeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1792 katika nchi za Ulaya na Marekani. Katika kipindi hiki mwanamke hakuthaminiwa katika jamii yake na alikuwa ni mtu wa daraja la chini. Vilevile wanawake hawakuhusishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile siasa na uongozi. Mwanamke alionekana kuwa nafasi yake ni jikoni. Unyanyaswaji huu ndio ulisababisha kuibuka kwa nadharia ya Ufeministi. MacKinnon (keshatajwa) alieleza sababu za kuibuka kwa nadharia hii ya Ufeministi ni pamoja na mwanamke kutawaliwa na mwanaume kama kundi na pia mtu mmoja mmoja. Pili, mwanamke amefanywa awe tegemezi katika jamii na siyo kwasababu za asili au kibailojia. Tatu, mgawanyo wa majukumu ambao unahusisha jinsia unamuweka mwanamke katika kiwango cha juu cha kazi zisizo na hadhi. Wafula (2002) anaeleza kuwa A Vindization of the right of a woman (1792) ya Mary Wollstonecraft ni miongoni mwa kazi za mwanzo kufafanua masuala ya wanawake kinadharia. Chapisho lingine ni The Second Sex (1952) ya de Beauvoir (1949) ambalo lilikosoa na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha au kumdunisha mwanamke, kama vile dini, ndoa na utamaduni.

Msingi mkuu wa Nadharia ya Ufeministi ni uwakilishaji wa haki za mwanamke kufuatana na kuambatana na imani ya usawa wa kijinsia, inayojaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii ambayo inahusishwa na sababu za kimaumbile. Wafula & Njogu (2007) wanaona kuwa Nadharia ya Ufeministi inaongozwa na misingi kadhaa. Kwanza, kutumia fasihi kama jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali ya mwanamke. Pili, nadharia hii inanuia kuleta usawa wa kijinsia na kitamaduni kupitia kwa miundo misingi inayopatikana katika jamii. Inapigania jamii mpya inayoheshimu jinsi ya kike kupitia kwa amali zake. Tatu, kuhamasisha utungaji wa kazi za kisanaa zenye muhusika wa kike anayeweza kuigwa ambaye hamtegemei mwanamume ili wajulikane. Mwisho, ni kuzindua mwamko kwa upande wa mwanamke jinsi anavyojiona, kuvumbua na kuziweka wazi kazi za fasihi zitungwe na mwanamke.

Kwa mujibu wa de Beauvoir (1949) utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Baada ya kukubali hali hiyo, mwanamke anaishia kuwa chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni huo. Naye, Barrett (1988) anaongeza kuwa Nadharia ya Ufeministi ni dhana inayoeleza nia na lengo la mwanamke anayedai kujitetea katika jamii mbalimbali.

Mawazo ya dhana hii ni kupinga mfumodume na kutafuta suluhisho juu ya changamoto zinazomkabili mwanamke katika jamii zinazoongozwa kwa mawazo na hisia za wanaume. Mtafiti ameamua kutumia Nadharia Ya Ufeministi kwa sababu inabainisha namna mwanamke anavyosawiriwa katika jamii na hivyo imemsaidia mtafiti kubaini vipengele vya kuchunguza kuhusiana na usawiri wa mwanamke katika diwani iliyotungwa na mtunzi mwanamke.

## 3. Mbinu za Utafiti

Makala hii imechunguza jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Makala imetokana na utafiti wa kimaktaba. Mbinu ya usampulishaji lengwa ndiyo iliyotumika katika kuteua Diwani ya Kurunzi ya Rose Mbijima kwa kuwa ni diwani iliyoandikwa na mtunzi mwanamke nchini Tanzania. Diwani hii pia inatumika kufundishia viwango mbalimbali vya elimu vikiwemo vyuo vikuu. Data za makala zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na uhakiki wa diwani teule. Mtafiti aliisoma diwani teule ya Kurunzi, kisha kufanya uchambuzi na uhakiki kuhusu usawiri wa mwanamke. Kupitia usomaji huo, mtafiti alipata taarifa zinazohusiana na kusudi la makala. Katika makala hii, data zimechambuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Mchakato wa uchambuzi ulihusisha, nukuu za mashairi yanayomsawiri mwanamke ili kupata data zilizokusudiwa. Uchambuzi pia uliongozwa na Nadharia ya Ufeministi hasa katika kubaini makundi ya ubaguzi dhidi ya wanawake.

### 3.1. Dibaji ya Diwani ya Kurunzi ya Rose Mbijima

Diwani ya Kurunzi ni kitabu chenye mkusanyiko wa mashairi ya Rose Mbijima kilichoandikwa mwaka (2019) na kuchapwa na Moccony Printing Press, Dar es Salaam. Diwani ya Kurunzi, kifani, imesheheni lugha ya ishara, picha, mafumbo na hata istiara. Aidha, mashairi yana maumbo na urari wenye ubunifu. Kimaudhui mashairi haya ni kurunzi inayomulikia masuala ya siasa, malezi, uchumi, ufisadi, ndoa, dini na hata TEHAMA. Kwa ufahamu wangu Diwani ya Kurunzi inaleta katika ulimwengu wa fasihi mada mpya ambazo hazijawahi kujadiliwa kwa undani na washairi wa awali wa Kiswahili.

## 4. Uchanganuzi wa Data na Matokeo ya Utafiti

Data za makala hii zinaonesha kuwa, mwanamke amesawiriwa katika mitazamo miwili muhimu. Kwanza, mwanamke amesawiriwa kitamaduni na pili, amechorwa kisasa. Rodney (1972) anaeleza kuwa majukumu kwa wanajamii katika jamii nyingi ulimwenguni, hasa za Kiafrika, yamegawanywa kufuatia hali ya uana na pia kwa kuzingatia utamaduni wa jamii husika. Anaendelea kueleza kuwa kipindi cha historia pia huwa na mchango katika kugawanya majukumu. Data zilizopatikana zimetumika katika kuonesha namna mwanamke alivyosawiriwa kimapokeo na kisasa katika jamii yake. Aidha, data zinaonesha kuwa mwanamke ni mtu ambaye huweza kuvaa uhusika zaidi ya kuwa mama na mke nyumbani, mwenye uwezo wake wa kiutendaji na aliyefungwa ndani ya mipaka na matakwa ya mme wake. Makala hii inafafanua usawiri wa jinsi ya kike kimapokeo na kisasa kwa mtazamo chanya na hasi.

### 4.1. Mtazamo wa Kimapokeo Kuhusu Mwanamke

Baada ya uchanganuzi wa data uliofanyika, matokeo yanaonesha kuwa mwanamke katika Diwani ya Kurunzi amechorwa katika mtazamo wa kimapokeo katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji. Katika makala hii, dhana ya kimapokeo inarejelea mambo yote yaliyomuhusu mwanamke kabla ya kuanza kwa vuguvugu la kudai usawa wa kijinsia. Diwani hii imeonesha kuwa yangali mambo mbalimbali ya msingi ambayo mwanamke hana budi kuyafanya bila kujali kiwango cha ustaarabu alichokifikia kutokana na maendeleo yaliyopo katika jamii.

Katika shairi la Wasikilize tunaelezwa nasaha anazopewa kichuna na mume wake. Mwandishi anatumia jina ‘kichuna’ kumrejelea mwanamke aliyetolewa kijijini na kuletwa mjini kama mke. Jambo hili la kutafuta mke linaonesha kuwa huenda zipo jamii ambazo zina mtazamo kuwa suala la kuoa ni vyema kulifanyia nyumbani. Katika ubeti wa tano mwandishi anasema:

> Mabonde nimevuka, mito nimeongelea,
> Kwa uhodari mkubwa, milima nikaipanda,
> Sifa wakanisifia, kila jina nikaitwa,
> Tega sikio kichuna, tuliza wangu mtima. Uk 12

Katika ubeti huo mwanaume anaeleza namna ilivyomgharimu kumtafuta mwanamke wa maisha yake. Ubeti huu unadhihirisha wazi kuwa mwanamke ni mtu ambaye hutafutwa sehemu yoyote na mwanaume anapohitaji kuoa. Jambo hili, linadhihirisha kuwa mwanaume ndiye mwenye uchaguzi na maamuzi ya kupenda na kisha kuoa, na si mwanamke. Matokeo haya yanaonesha kuwa katika suala la ndoa bado jamii zinaamini katika mfumo dume. Matokeo haya yanakinzana na mtazamo wa Gicuku (2012) anayeeleza kuwa asasi hii haina budi kubadilika kwa kuzingatia namna dunia ya sasa ilivyo kuliko kung'ang'ania ukale ambao unasemekana ndio mzuri ilhali kuna mengi yamebadilika na mengine yanaendelea kubadilika. Hivyo kubadilika kwa utamaduni huu katika jamii nyingi, unasababisha wanawake wengi kutokuwa waoga kueleza hisia zao wakati wanapompenda mwanaume na kuhitaji kuolewa naye.

Pia, data zinaonesha, kupitia mhusika mwanaume, zinafunua nafasi nyingine ya mwanamke kama mlezi bora wa familia. Lengo la mwanaume kuoa ni kuhakikisha anampata si mwanamke tu, bali mwanamke ambaye atakuwa mama bora kwa familia yake. Katika ubeti wa tisa wa shairi la Wasikilize mwanaume anamueleza kichuna wake maneno haya;

> Lea yako familia, imarisha yako nyumba,
> Yasafishe mazingira, wakuite mama bora,
> Kuwa ruwaza kichuna, milele nitakupenda,
> Tega sikio kichuna, tuliza wangu mtima. Uk 12

Ubeti huu umejaa nasaha na ahadi kutoka kwa mwanaume kwenda kwa kichuna. Maneno haya yanaonesha kuwa mwanamke anao wajibu wa kuhakikisha anakuwa mfano bora wa kuigwa katika jamii yake, kwa kutekeleza wajibu wake wa kulea familia yake. Majukumu hayo yanapofanywa kwa ufasaha

humfikisha mwanaume katika kilele cha furaha na matamanio yake ya kuwa na mke bora. Hivyo, humlipa upendo kama tunu kwa kufanikisha furaha yake, jambo ambalo kwa hakika linamuondoa mwanamke katika nafasi ya kufanya vitu kwa utashi wake bali kwa ajili ya heshima ya mwanaume. Matokeo haya yanawiana na yale ya Yego (2013), anaposema kuwa mwanamke ndiye chemichemi ya maisha. Pia, ndiye mlezi wa watoto; ndiye humwongoza mtoto maishani mwake. Anaendelea kueleza kuwa mwanamume anatunzwa kama mtoto. Hivyo taswira ya malezi ya mume kama mtoto yametumika kuchora picha ya mwanamume kama kiumbe dhaifu na ambaye anahitaji kutunzwa kwa uangalifu. Kwa upande mwingine, umuhimu wa mwanamke kama mlezi hauwezi kupuuzwa.

Vilevile, mwanamke anaendelea kusawiriwa kama mshauri wa watoto katika familia. Jukumu hili muhimu tangu enzi, linaonekana kuendelea kukasimiwa kwa wanawake katika jamii. Jamii inaendelea kuamini kuwa tabia njema za watoto au vijana hutokana na wanawake kutimiza majukumu yao ipasavyo na siyo kinyume chake. Mtunzi anaikumbusha jamii inayozungumzia usawa wa kijinsia katika nyanja zote kuwa wajibu wa kutoa ushauri ni jukumu muhimu linaloelekezwa kwa akina mama. Mtunzi anaeleza katika shairi la “mgogoyo” kuwa:

> Mwanangu nakuusia, usinitoe manani,
> Acha kupuyanga puyanga, chuo sawa na bahari,
> Sifa zake wazijua, itakumeza bahari,
> Mwanangu nakuusia, usinitoe manani. Uk 20

Ubeti huu unadhihirisha kuwa ushauri na nasaha za wazazi hasa mama ni kitu muhimu katika mafanikio ya mtu yeyote. Jambo hili ni la kimapokeo licha ya ukweli kuwa hata sasa bado linaendelea kwani maisha ya mwanadamu yanahitaji nasaha na halina mwisho. Mwandishi anaonesha msisitizo wa mzazi katika mshororo wa kwanza na wa mwisho katika ubeti huo juu ya hofu yake kwa mwanae. Mama kama mzazi anatamani mwanae akumbuke na kuhakikisha kuwa ushauri anaompatia haumtoki kamwe katika moyo wake. Mtunzi anaikumbusha jamii kuwa suala la kutoa nasaha na makatazo ni endelevu kwa wanawake wa zama zote. Pia, halina mipaka wala ukomo wa kutolewa, mathalani mtunzi anamtumia kijana ambaye yuko katika umri wa kuanza chuo kama mfano kuwa ushauri na nasaha za wazazi hazina ukomo. Aidha, matokeo haya yanaungwa mkono na Kimondiu (2019) katika utafiti wake anaposema kuwa suala la kutoa ushauri mwema lina umuhimu mkubwa katika kuijenga familia na jamii kwa jumla. Ushauri mwema hurutubisha jamii yoyote kwa ukamilifu. Mathalani kupitia wimbo wa Bosco Mulwa wa Mother (mama) mwanamke amesawiriwa kama mshauri mwema. Mama yake alimtahadharisha na dunia ambayo imejaa maovu na misukosuko. Alimweleza umuhimu wa kuvumilia kwa kumwambia kuwa, mtu anapovumilia hatimaye hufanikiwa. Hii ni sifa nzuri anayopewa mama kuonesha kuwa, wanawake wanajua wajibu wao. Katika nyimbo alizozitafiti Kimondiu (2019), imebainika kuwa mwanamke ana uwezo mkubwa wa kushauri juu ya msingi bora wa maisha na tahadhari kuhusu mambo ya ulimwengu yanayoweza kumletea mtu balaa baadaye.

Pia, mwandishi katika shairi la Asante mama anapigilia msumari wa kimapokeo kuwa mama ndiye mtu wa thamani sana duniani. Mtunzi anatukumbusha hilo pale anapotoa shukrani zake kwa mama yake kwa malezi bora ambayo kwa hakika hawezi kuyalipa. Mtunzi anaonesha kuwa mama katika kutimiza wajibu wake wa malezi kuna nyakati ambazo alilala bila kula, alikesha wimawima na hata mwili wake kugeuzwa kuwa msala. Mambo haya kama yalivyooneshwa na mtunzi yanaweza kufanywa na mama pekee. Mtunzi katika ubeti wa tano anaonesha ukubwa wa nafasi ya mama katika malezi anasema;

> Hata nijenge ghorofa, Kilimanjaro mlima,
> au nikupe dunia, pande zote kutawala,
> Haviwezi thaminika, ulotenda kufikiwa,
> Nikulipe nini mama? Sinacho cha kukulipa! Uk 1

Katika ubeti huo wa tano ni dhahiri kuwa mwanamke amepewa nafasi ya juu sana kwa sababu ya kutimiza wajibu wake wa kimalezi kwa watoto wake. Nadharia ya Ufemenisti katika muhimili wa pili unaolenga kuleta usawa wa kijinsia na kitamaduni kupitia kwa miundo misingi inayopatikana katika jamii, unaeleza kuwa jamii ina miundo misingi yake ambayo hugawa majukumu kwa kuzingatia jinsi. Hivyo data hii inaonesha kile kinachoelezwa kwenye nadharia kuwa miundo iliyopo inawapatia wanawake majukumu ya nyumbani na wanaume uhuru wa kutoka na kutafuta kwa ajili ya familia. Matokeo haya yanafanana na yale ya Mwangi & Kamwara (2025) kuhusu suala la malezi, wanaposema kuwa malezi ya watoto katika jamii nyingi za Kiafrika limeachwa kwa mwanamke. Anafaa kulitekeleza hili pasi na kulalamika. Mwanaume huwa hahusishwi katika malezi. Yeye ana uwezo wa kuondoka na kurudi nyumbani bila kuulizwa, kwani kulingana na itikadi ya jamii hizi mwanamume ndiye kiongozi wa familia na hivyo hapaswi kuhojiwa kwa kile akitekelezacho. Matokeo haya hayadhihirishi nafasi ya mwanaume (baba) katika malezi kabisa licha ya kuwa jitihada nyingi zinafanywa naye kuhakikisha ustawi wa familia yake. Hivyo, mwanamke na mwanaume wote wana uwezo sawa wa kimalezi na watakaposhirikiana kwa pamoja jamii itakuwa na watu bora waliopata malezi bora kutoka kwa wazazi wote.

#### *4.1.1. Mtazamo Hasi wa Kimapokeo Kuhusu Mwanamke*

Mtafiti amebaini kupitia data za makala hii kuwa mwanamke amechorwa kuwa na sifa hasi na ambazo ni za kimapokeo. Data zinaonesha kuwa mwanamke bado anahusishwa na sifa mbaya katika jamii kama vile chanzo cha uovu. Hili linajidhihirisha katika shairi la Mgogoyo ambapo mwanamke amechorwa kama kiumbe mlaghai ambaye anahatarisha usalama na mafanikio ya kimasomo ya mwanaume. Mtunzi anaonesha jinsi mzazi anavyomuasa mwanae wa kiume katika safari yake ya masomo ya chuo kikuu, kama ifuatavyo:

> Ogopa ukajitenge, jiepushe na nisai,
> Watakurudisha nyuma, kimasomo na kiuchumi,
> Bahari itakumeza, ukavuliwa ma’nani,
> Mwanangu nakuhusia, usinitoe maanani. Uk 20

Katika ubeti huu, mwanamke anahusishwa na sifa za kutisha, kama vile kiumbe cha kuogopa kukutana nacho ikiwa utahitaji kufanikiwa katika taaluma na uchumi. Mwanamke anapewa sifa ya ufilisi wa fedha kwa mwanaume. Hivyo rai ya mtunzi ni kuwa ikiwa mwanaume atahitaji kufanikiwa, basi anapaswa kujiweka mbali na mwanamke. Matokeo haya yanafanana na yale ya Mutua (2017) anayesema kuwa wanawake wengi wamesawiriwa kama wazururaji mijini huku wakiwanyakua mabwana wa wenzao, kulewa na kufanya ukahaba. Wanawake wanasawiriwa kama wanaopenda anasa, dhulumati wa ndoa, na wachochezi wa wanaume kushiriki ulevi na umalaya. Mtazamo huu unaonekana kumpa mwanamke sura mbaya katika jamii licha ya ukweli kuwa wapo wanawake ambao hawawategemei wanaume kimaisha. Hata hivyo hawaondoi sifa ya uwapo wa wanawake wema ambao ni msaada kwa wanaume katika masuala ya kiuchimi na elimu.

### 4.1.2. Mwanamke kama Chanzo cha Uonevu Dhidi ya Jinsi Yake

Mtunzi katika shairi la Mtetezi wao anamchora mwanamke kama chanzo cha ukatili dhidi ya watu wengine wa jinsi yake. Katika ubeti huu, mtunzi anakemea kwa dhati tabia zinazofanywa na wanawake dhidi ya wafanyakazi katika nyumba zao. Mwandishi anaonesha kuwa wanawake wenyewe ndio sababu ya kukatisha ndoto za kielimu za wasichana wengi kwa kuwaleta mjini kufanya kazi za ndani kama anavyosema katika ubeti wa pili.

> Vijijini kuwatoa, mjini tunawaleta,
> Ahadi kuwamwagia, pesa nene watalipwa,
> Shuleni kuwaipua, kwa ushawishi mkubwa,
> Sisi ni chanzo cha yote, tubadilike tabia. Uk 60

Ubeti huo, unaeleza namna mwanamke anavyokatili maendeleo ya mwanamke mwenzake. Wanawake wamekuwa vinara wa ushawishi kwa kuwaachisha masomo wasichana wenye umri mdogo kutoka maeneo mbalimbali ya vijijini na kuwaleta mjini kufanya kazi za ndani. Kama anavyoeleza, maisha magumu ya vijijini ni chanzo kikuu cha kufanikisha urubuni unaofanywa na wanawake hao. Hivyo, mabinti wadogo wanashawishika kwa fedha wanazoahidiwa kuja kupewa mjini, hali inayokatisha ndoto zao za kielimu.

Aidha, mwanamke anaonekana katili zaidi kwa kudhalilisha na kuvunja haki za binadamu kwa wasichana wanaowaleta mjini. Mtunzi katika ubeti wa nne wa shairi la mtetezi wao anasema:

> Mjini wakifikishwa, mitaji wanageuzwa,
> Wanaume kutafutiwa, kwafedha kuwanunua,
> Pasi huruma twatenda, uliokithiri unyama,
> Sisi ni chanzo cha yote, tubadilike tabia. Uk 60

Katika ubeti huu, mtunzi anakemea tabia mbaya na ya kikatili ya kuwageuza wasichana wadogo kuwa kitega uchumi. Jambo hili si jema kulisikia likitendwa na wanawake ambao wamepambwa kwa sifa ya umama, ulezi wa familia na kioo cha nyumba kama alivyojieleza katika ubeti wa kwanza wa shairi hili. Wanawake wanaotekeleza shughuli hizi za kikatili na kidhalilishaji katika jamii hawafai kuigwa katika jamii. Matendo haya yanadhihirisha kuwa adui wa mwanamke ni mwanamke mwenzake aliyekosa utu.

Sambamba na hayo, mwanamke anaonekana kuwa kiumbe asiye na upendo wala kujali. Katika shairi la Mtetezi wao ubeti wa nne hadi saba, mtunzi anaonesha tabia za kutojali na zisizodhihirisha upendo kabisa kwa wafanyakazi zinazofanywa na wanawake. Mtunzi anasema kuwa wafanyakazi wamekuwa wakifanyishwa kazi bila kupata muda wa kupumzika, wanageuzwa kuwa ombaomba barabarani, wanashinda bila kula licha ya kazi ngumu wanazofanya. Mwandishi katika ubeti wa sita anasema:

> Tumegeuka wanyama, tukiwatesa mayaya,
> Mishahara kutowapa, hatuwalipi kwa muda,
> Miezi miwili mpaka, miezi juu ya sita,
> Sisi ni chanzo cha yote, tubadilike tabia. Uk 60

Mtunzi katika ubeti huo anatuonesha namna wanawake walivyo chanzo cha ukatili dhidi ya wanawake wenzao. Licha ya mambo yote wanayotendewa wafanyakazi kama yalivyoelezwa bado wanashindwa kulipwa hata stahiki zao kwa wakati. Tabia hizi ni mbaya kutekelezwa na mwanamke ambaye ni mfano wa kuigwa na mjenzi wa jamii yenye kujali haki, upendo na usawa kwa kila mtu. Usawiri huu wa mwanamke unadhihirisha kuwa uwezo alionao mwanaume wa kutenda matendo mema au maovu, unapatikana pia hata kwa wanawake katika jamii.

## 4.2. Mtazamo wa Kisasa Kuhusu Mwanamke

Katika mtazamo wa kisasa, mtunzi wa Diwani ya Kurunzi amemsawiri mwanamke kwa mtazamo mpya zaidi ukilinganisha na ule wa kimapokeo. Data zinaonesha kuwa mwanamke ameongezewa uwezo katika nyanja mbalimbali za maisha yake na mahusiano yake na jamii inayomzunguka. Mtunzi amemsawiri mwanamke kama mwanamapinduzi. Huyu ni mtu ambaye huleta mageuzi au mapinduzi katika nyanja mbalimbali za maisha yanayomzunguka. Kwa mfano, katika shairi la Maisha ya ndoa mtunzi anamchora mwanamke katika mtazamo wa kimapindunzi ambaye anapinga mfumo dume katika ndoa. Mwanamke anauvunja ukimya wa muda mrefu wa kukubali na kutii kila kitu kutoka kwa mume. Mshairi anajaribu kumuweka wazi jinsi mwanamke wa kisasa anavyowaza na kuhitaji kutendewa katika maisha ya ndoa. Katika ubeti wa nne wa shairi la "Maisha ya ndoa", wanamke anamueleza mwanaume ifuatavyo:

> Mme tega masikio, nisikilize kwa makini,
> Majukumu nayajua, jikoni hadi chumbani,
> Kuchapana zilipendwa, ndoa sio utumwa,
> Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije? Uk 17

Katika ubeti huu, mwanamake anamtahadharisha mume wake kuhusu mienendo ya kimazoea ya kuwapiga wanawake na kuwatumikisha katika ndoa. Mwanamke anapaza sauti na kupinga vikali suala la kupigana katika ndoa kwa sasa. Aidha, katika mshororo wa nne wa ubeti, anawashangaa watu wengine wanaoishi katika maisha ya kale ya kukubali utumwa ndani ya ndoa. Suala la ndoa

katika jamii ya sasa linapinga na kukemea masuala yote yanayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia katika ndoa. Wanawake kwa wanaume wanasimama kidete kupinga na kuchukua hatua dhidi ya watu wote wanaotekeleza vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake. Mathalani katika nchi ya Tanzania, madawati mengi ya jinsia yamefunguliwa kila sehemu ya nchi ili kuhakikisha kuwa ukatili na unyanyasaji wa wanawake unakomeshwa.

Aidha, mtunzi katika shairi hili anamtumia mhusika mke kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusu matamanio ya wanawake katika ndoa. Katika ubeti wa nane hadi wa kumi katika shairi hili, yanatajwa mambo ambayo mwanamke anatamani yafanyike katika ndoa mathalani kusaidiwa majukumu kama vile kuchota maji. Hali hii itamsaidia mwanamke kuwa mtulivu na mwenye kujituliza nyumbani. Pili, katika ubeti wa tisa, mshororo wa kwanza na pili, mshairi anaonesha kuwa mwanamke anahitaji kudekezwa na kubembelezwa:

> Mwanamke ndege njiwa, apetiwe peti peti,
> Asiguswe kwa mabaya, atapeperuka mbali. Uk 17

Mtunzi anaeleza hapa kuwa mwanamke anahitaji maneno laini, na kukingwa na hatari zote kutoka ndani. Mwanamke anafananishwa na njiwa arukaye kwenda mbali pindi anapokabiliwa na hali hatarishi nyumbani. Mwanamke huyu anapaza sauti juu ya mapinduzi ndani ya nyumba ili kuhakikisha ndoa zinakuwa bora na salama kwa kila mwanandoa. Aidha katika ubeti wa kumi, mwanamke anapaza sauti juu ya mfumo dume katika ndoa, pale anaposema:

> Wanaume mwachekesha, madaraka punguzeni,
> Uwapo nyumbani pika, ndoa zipalilieni,
> Saa zipi nitapika, mimi wewe tu kazini?
> Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije? Uk 17

Katika ubeti huu, mwanamke anahitaji usawa katika utekelezaji wa majukumu nyumbani. Katika karne hii ambayo mwanaume na mwanamke wana haki sawa katika ajira, ni muhimu kusaidiana kwani wote wanakuwa kazini. Jambo hili ambalo analieleza ni ishara ya kimapinduzi kwa mfumo uliozoeleka katika jamii nyingi za kiafrika. Bila kujali kiwango cha elimu na ustaarabu ambao mtu binafsi ameufikia, mtazamo wa jamii ni kuwa shughuli nyingi za nyumbani, hasa kupika, ni jukumu la mwanamke. Hivyo, kupinga suala hili hadharani ni ushahidi kuwa wanawake, katika karne hii ya 21, wanahitaji usawa na usaidizi katika mambo mbalimbali ambayo awali jamii iliyaelekeza kwa mwanamke, bila kujali majukumu yake mengine aliyobebeshwa na jamii yake. Mapinduzi haya yanaashiria kuwa mwanamke anatamani usawa katika utendaji kama ilivyo kwa mwanaume.

Pia, katika shari la Nisai mwanamke anadhihirisha mtazamo mpya wa kimapinduzi juu ya suala la elimu kwa wanawake. Mshairi anaonesha kuwa mwanamke anahitaji kupewa haki ya kupata elimu kama ilivyo kwa mwanaume. Katika ubeti wa tatu, wa shairil la Nisai, mshairi anaonesha kuwa jinsi isiwe sababu ya kumzuia mwanamke kupata elimu:

> Elimu wajibu wetu, awali hadi vyuo,
> Jinsi sio ulemavu, wakitufungia ndani,
> Tusimame mnadabu, peke yetu twatosheni,
> Nisai sote muhimu, wagombezi wa jamii. Uk 4

Katika ubeti huu, mtunzi anatumia neno nisai kurejelea wanawake. Anaonesha kuwa wanawake wanahitaji kujisimamia wenyewe kuhakikisha kuwa wanapata elimu bora kuanzia elimu ya msingi hadi chuo kikuu. Aidha, mtunzi anakumbusha kuwa jinsi sio ulemavu (kama ilivyo kuwa ikitazamwa kimapokeo). Jamii ya sasa inapaswa kutambua kuwa elimu ni wajibu na haki ya msingi kwa wanawake wote kwa viwango vyote. Matokeo haya yanaungwa mkono na Salem (2013) anayeeleza kuwa hali za wanawake inakuwa mbaya kwa sababu hawana haki sawa na wanaume katika kumiliki rasilimali, ikiwemo elimu. Ijapokuwa siku hizi wazazi wengi wanawapa watoto wa kike nafasi ya kusoma, wangali wapo wazazi wasioona umuhimu wa kumsomesha mtoto wa kike. Hivyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa wanawake wote wanaungana kuhakikisha jambo hili linafanikiwa. Hii ni kwakuwa mwanamke na mwanaume wana uwezo sawa kiutendaji.

Aidha, katika ubeti wa tisa wa shairi la Nisai, mwanamke anaaswa kufanya mapinduzi katika suala zima la uongozi. Anaaswa kutafuta nafasi ya kuongoza na kufanya maamuzi kuanzia kiwango cha familia hadi ngazi ya nchi, kama ifuatavyo:

> Walikufanya bahau, ukageuzwa mlinzi,
> Nawe ukawa mtuvu, kunguru kwako hodari,
> Wakakuita ubavu, hufai madarakani,
> Nisai sote muhimu, wagombozi wa jamii. Uk 4

Mwanamke anawaeleza wenzake umuhimu wa kufanya mapinduzi ya kiuongozi kwa kuondokana na mitazamo ya kitamaduni inayomuona mwanamke kuma mlinzi wa nyumba na msaidizi tu wa mwanaume. Mtazamo huu, unaoshadidiwa na dini hubinya fursa ya mwanamke kuwa madarakani, ilhali ikimsaidia mwanaume katika kutekeleza shughuli zote za kiutawala. Hivyo, katika ubeti wa kumi wa shairi la Nisai, mwanamke anatoa wito kwa wanawake wafanye jitihada kuhakikisha kuwa wanashika hatamu za uongozi:

> Nasi tushike hatamu, tuwemo uongozini,
> Tusiwe wapendelevu, kuendekeza nafsi,
> Ni bora tuwe hashimu, walafi wasweke ndani,
> Nisai sote muhimu, waombozi wa jamii. Uk 4

Katika ubeti huu, wanawake wanahamasishwa kushika hatamu mbalimbali za uongozi katika jamii. Wanaaswa kuepeuka tamaa binafsi ili waweze kuwa viongozi bora na pia kuhakikisha wanatekeleza wajibu, ukiwemo kulinda rasilimali za nchi na kuhakikisha walafi wanahukumiwa. Hivyo, mtazamo huu unadhihirisha dhamira ya kweli ya kimapinduzi waliyonayo wanawake wa kisasa kuhusu haki yao ya kuwa viongozi na kufanya maamuzi sawa na yale wanayofanya wanaume. Mawazo haya yanaunga mkono muhimili wa nadharia ya Ufeministi unaolenga kuzindua mwamko kwa upande wa mwanamke jinsi anavyojiona kwa kushiriki katika shughuli zote ambazo anaweza kufanya bila kujali jinsi yake.

Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kuwa nafasi ya mwanamke katika jamii inasawiriwa kwa mtazamo hasi na mtazamo chanya bila kujali kuwa usawiri huo unafanywa na mtunzi wa kiume au wa kike. Mathalani katika Diwani ya Kurunzi, mwanamke amesawiriwa kwa mtazamo chanya kama mlenzi, mshauri na mwanamapinduzi. Aidha, mtunzi amemsawiri kwa mtazamo hasi kama vile mtu katili, asiye na huruma na kujali, asiye na upendo na mvunjaji wa haki za binadamu, hasa kwa watoto wa jinsia ya kike. Matokeo haya yanawiana na yale yaliopatikana katika tafiti zilizopita (Ali, 2014; Abdalla, 2020; Salem, 2013), ambazo zilieleza kuwa mwanamke amechorwa kwa mtazamo hasi na chanya katika jamii kupitia kazi za fasihi hususan nyimbo mbalimbali. Hivyo, matokeo ya utafiti huu na ya tafiti tangulizi yanaonesha kuwa mwanamke anasawiriwa katika kazi zilizoandikwa na watunzi wanaume na wanawake kwa hali chanya na hasi.

Aidha, matokeo yanaonesha kuwa mwanamke anapiga hatua katika kujikomboa kutoka kuwa mtu tegemezi kwa mwanamume na kuanza kujisimamia katika nyanja mbalimbali za kimaisha. Mtunzi anamsawiri mwanamke wa kisasa kama mwanamapindizi ambaye anapambana kupata nafasi sawa na mwanamume katika elimu, ndoa, uchumi na uongozi. Mwanamke anasawiriwa kama kiumbe mwenye nguvu, maono, akili na uwezo wa kutoa hoja na kuitetea mbele ya jamii bila kujali jinsia yake. Vilevile, mwanamke anaonekana kuwa na jukumu la malezi na ushauri kwa watoto katika jamii, wajibu unaompatia mwanamke nafasi kubwa katika kushiriki kuwajenga watu bora. Matokeo haya yanafanana na yale ya Limbe (2024) yalionesha kuwa mwanamke wa kisasa ni mwenye nguvu ya uchumi, aliyejikomboa kielimu, na mwenye uwezo wa kujisimamia na kuisaidia jamii bila utegemezi. Aidha, mwanamke mwenye nguvu kubwa kiuchumi na kielemu, anamtisha mwanaume, na kumfanya tegemezi na dhaifu kwa mwanamke

## 5. Hitimisho

Makala hii ililenga kubainisha jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika Diwani ya Kurunzi. Uchambuzi wa data umeonesha kuwa zipo sifa mbalimbali za kimapokeo alizopewa mwanamke zinazofaa kuendelezwa kama vile kuwa mama bora wa familia, mshauri na mlezi wa familia. Aidha, uchambuzi umeonesha kuwa mtunzi wa Diwani ya Kurunzi ameonesha mabadiliko katika nafasi ya mwanamke katika jamii. Mtunzi amemchora mwanamke wa kisasa kama mwanamapinduzi katika kutaka usawa katika nyanja mbalimbali za kijamii: ndoa, elimu na uongozi. Hata hivyo, mtunzi hakuona haya kuonesha udhaifu wa mwanamke licha ya kuwa yeye ni mwanamke. Mtunzi amekemea tabia mbaya na matendo maovu yanayotendwa na wanawake katika jamii. Mtunzi amemsawiri mwanamke kama chanzo cha uovu katika jamii na pia sababu ya kukwamisha maendeleo ya jinsi yake katika nyanja mbalimbali za maisha. Matokeo haya yanaonesha kuwa mwanamke si tu anachorwa katika nafasi hasi na watunzi au wahakiki wa kiume bali watunzi wanawake anaweza kufanya hivyo pia. Makala hii, inapendekeza kuwa kazi za watunzi wa kike wa ushairi ziendele kutafitiwa zaidi ili kuchochea mabadiliko makubwa juu ya mtazamo hasi kuhusu mwanamke na nafasi yake katika jamii.

## Marejeleo


Abdalla, S. S. (2020). Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Kidumbaki Zanzibar (Doctoral dissertation, SUZA). University Press.

Ali, E. (2014). Kutathimini nafasi ya mwanamke katika mashairi ya Kiswahili: Uchunguzi wa mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyapala: (Tasnifu ya Shahada ya uzamili ya Kiswahili Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Barrett, M. (1988). Women's Oppression Today: The Marxist Feminist Encounter. London Verso.London.

Challigha, N. E. (2011). Usawiri wa Mwanamke na Mgawanyo wa Majukumu Kijinsia katika Fasihi Picha ya Katuni Mnato za Kiswahili. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

De Beauvoir, S. (1949). The second sex (C. Borde & S. Malovany-Chevallier, Trans.). Knopf/Random House LLC.

Gicuku, M. (2012).Usawiri wa maudhui ya ndoa katika Ushairi wa Euphrase Kezilahabi na kithaka wa Mberia. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Indede, F. (2011). Mwanamke Angali Tata Katika Ushairi wa Kisasa? Swahili forum 18: 163-197

Kimondiu, D. K. (2019). Usawiri wa Mwanamke Katika Nyimbo za Sifo za Wakamba. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Machakos Institutional Repository. (Haijachapishwa)

Limbe, Z. D. (2024). Usawiri wa Wanawake wenye Uwezo katika Muziki wa Bongo Fleva nchini Tanzania. Mwanga wa Lugha, 9(1), 33-41.

Lyatuu, J. (2011). Usawiri wa Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na Kiume: Uchaguzi katika Riwaya Teule. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

MacKinnon, C. A. (1991). Toward A feminist theory of the state. London. Havard University Press.

Mbijima, R. (2019). Kurunzi. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mutua, J. M. (2017). Mtazamo wa waandishi wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Pwani (Haijachapishwa)

Mwakanjuki, N. (2022). Mapungufu ya Kiutamaduni Yanavyoathiri Ustawi wa Mwanamke katika Jamii: Mifano Kutoka Riwaya ya Sikujua. Jarida la Fahari ya Kiswahili, 1(1), 115 – 130.

Mwangi, M. N. & Kamwara, K. (2025). Jinsia ya Mtunzi na Usawiri wa Wahusika katika Riwaya za Kiswahili: Nyuso za Mwanamke na Nguu za Jadi. East African Journal of Swahili Studies, 8(1), 410-423. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3131.

Ngaiza, M. K. (2004). Harmonisation and mainstreaming gender in local government or transforming patriarchy: the case of two wards in Bukoba District Council, Tanzania. Tanzanian Journal of Development Studies. 5: 25-38.

Rodney, W. (1972). How Europe Underdeveloped Africa. London: Rogle-L'Ouverture Publishers.

Salem, B. M. (2013). Usawiri wa Jinsia Katika Lugha ya Mashairi: Mifano kutoka Mashairi ya Shaaban Robert (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Schipper, M. (2006). Never Marry a Woman with Big Feet: Women in Proverbs from Around the World. Amsterdam: Amsterdam University Press.

Wafula, R. M. na Njogu K. (2007). Nadharia za uhakiki wa fasihi, Nairobi. Jomo Kenyata Foundation.

Wafula, R. M. (2002). "My Audience Tells me Which Tongue I Should Sing in: The Politics About Languages in African Literatures", Political Independence with Linguistic Servitude: The Politics About Languages in the Third World (ed. Samuel Obeng & Beverly Hartford). New York: Nova Science Publishers.

Yego, E. K. (2013). Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarabu za Zanzibar. Tansifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Paris: Minuit.